

ZAIDI YA CECIL:

# SIMBA WA AFRIKA HATARINI

# YALIYOMO

## KUHUSU PANTHERA

Panthera, iliyoanzishwa mwaka 2006, imejitolea kuhifadhi jamii ya paka mwitu na nafasi yao muhimu katika ikolojia ya dunia. Timu ya Panthera yenye wanabayolojia wenye weledi, wataalamu wa masuala ya sheria na wanaharakati wa masuala ya paka mwitu hutengeneza mikakati ya kibunifu kulingana na zana za sayansi zilizopo kuwalinda duma, chui, mbwa mwitu, jagwa, simba, chui wa kwenye barafu, na simba marara pamoja na mazingira yao, Katika nchi 50 duniani, Panthera inafanya kazi na wadau mbali mbali kupunguza ama kuondoa kabisa vitu vinavyotishia paka mwitu—hivyo kuhakikisha maisha yao, na yetu. Tembelea **panthera.org**

## KUHUSU WILDAID

Misheni ya WildAid ni kutokomeza biashara haramu ya wanyama pori katika uhai wetu. Tunaona dunia ambayo watu hawana tena haja ya kununua bidhaa za wanyamapori kama vile mapezi ya papa, pembe za ndovu na za faru. Tukiwa na rekodi isiyomithilika ya mabalozi maarufu na mtandao wa kidunia wa vyombo vya habari  washirika, WildAid hutoa aghalabu Dola za Kimarekani Milioni 200 za michango kila mwaka kwa vyombo vya habari huku kukiwa na ujumbe mwepesi lakini mzito: “Tukiacha kuuza, na kuua kutakwisha”. Tembelea **wildaid.org**

## KUHUSU WILDCRU

Dk. David Macdonald alianzisha Kitengo cha Utafiti cha Uhifadhi wa Wanyamapori (WildCRU) mnamo mwaka 1986 katika Chuo Kikuu cha Oxford. Kwa sasa hivi kimekuwa ni kitengo kikubwa zaidi cha utafiti kilichopo kwenye chuo duniani na misheni yake ni kupata suluhu kwa matatizo ya uhifadhi wa wanyama pori kwa kufanya utafiti.  WildCRU inajulikana sana kwa kazi zake na wanyama wa jamii ya paka, ikiwemo tafiti za muda mrefu za simba na chui wa mabaka. Kituo chake cha mafunzo kwa wahifadhi wanaoanza kazi, kilicho mbali na nchi 32, hutengeneza wataalamu wazuri na viongozi wa baadae kwenye masuala ya uhifadhi. Tembelea **wildcru.org**

## WACHANGIAJI WA RIPOTI

Paul Funston
Philipp Henschel
Luke Hunter
Peter Lindsey
Katarzyna Nowak
Christina Vallianos
Karen Wood

Picha ya Cecil kwenye kava: Craig Taylor


| | |
|---|---|
| MUHTASARI | 1 |
| ATHARI YA CECIL | 2 |
| IDADI YA SIMBA | 4 |
| VITISHO | 6 |
| SULUHU | 15 |
| TAMATI | 23 |


## MAULIZO


**Panthera**
Karen Wood
8 West 40th Street, 18th Floor
New York, NY 10018
kwood@panthera.org

**WildAid**
Christina Vallianos
333 Pine St. Suite 300
San Francisco, CA 94104
vallianos@wildaid.org




Nick Garbutt

# MUHTASARI

Kuna hadithi chache sana za mnyama mmoja mmoja ambazo zimewahi kugusa dunia kama ilivyogusa hadithi ya Cecil, simba mzuri mwenye shungi nyeusi aliyewindwa kinyume na sheria Mwezi Julai Mwaka 2015 huko Zimbabwe. Masikitiko na hasira za watu wengi duniani zilipelekea kuwekwa kwa vikwazo vikali dhidi ya usafirishaji wa vipusa vya simba wa Kiafrika na ikaongeza vigezo vigumu zaidi kwa wawindaji na serikali kwa kuwataka watoe uthibitisho wa kisayansi kuhusiana na manufaa yanayosemekana wanayapata simba kwa kuwindwa.

Na muhimu zaidi, janga hili liliangazia dunia matatizo yanayowakumba simba wa Kiafrika, ambao muda si mrefu inajulikana kuwa watatoweka kabisa katika sehemu kubwa ya bara. Tofauti na imani zilizojikita, uwindaji wa kitalii ni tatizo dogo sana dhidi ya hatma ya simba wa Kiafrika — ni vita ndogo katika mapambano makubwa ya simba yaliyopeleka idadi yao kupungua kwa asilimia 43 katika kipindi cha miongo miwili hadi kufikia 20,000. Katika kipindi hicho hicho idadi za simba katika Afrika Magharibi, Afrika ya Kati na Afrika Mashariki zinasemekana kupungua kwa asilimia 60.

Kupotea kwa mazingira asilia ya simba kunakosababishwa na shughuli za kilimo ndio sababu kubwa inayochochea vitisho vingine dhidi ya simba. Huku wakiwa wamepoteza asilimia 75 ya mazingira yao asilia, katika kipindi cha miaka 100, sasa hivi simba wanakaa katika asilimia 8 ya mazingira yao asilia na inaripotiwa kuwa wametoweka katika nchi takriban 12 za Afrika.

Kadri jinsi idadi ya Waafrika inavyozidi kukua kila kukicha—kutoka Bilioni 1.2 hadi Bilioni 2.47 ifikapo mwaka 2050[1]—ardhi inahitajika zaidi ili watu wapate makazi na waweze kulima chakula cha kuwatosheleza. Ardhi inayotumika kwa kilimo katika nchi za chini ya Jangwa la Sahara inatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 21 na ardhi kwa ajili ya kulisha mifugo kwa asilimia 73 ndani ya kipindi hiki. Kadri jinsi makazi ya binadamu yanazidi kusogea kwenye uoto wa Savana, mwingiliano baina ya simba na binadamu utaongezeka. Simba watakuwa wanawania nafasi na mifugo katika Maeneo Yaliyohifadhiwa (PAs). Ukaribu na mifugo ya nyumbani unaweza kusababisha simba kuua mifugo, jambo ambalo linapelekea mauaji ya kisasi dhidi ya simba yanayofanywa na wafugaji pamoja na wafugaji. Hili ni moja katika matishio matatu katika Afrika Magharibi, ya Kati, Mashariki na baadhi ya sehemu za Afrika ya Kusini.[2] Nje na maeneo yanayolindwa, mauaji ya visasi na kuua kwa kujihami kunachukuliwa kuwa tishio kubwa kwa samba.[3]

> “
>
> **Simba wamepungua kwa asilimia 43 katika kipindi cha miongo miwili.**

Shughuli za kibinadamu pia zinapelekea uwindaji haramu wa nyama pori, tishio kubwa la pili dhidi ya simba na mawindo yao. Ijapokuwa zamani nyama pori ilikuwa inapatikana kama kitoweo kwa jamii zinazoishi porini, leo hii inauzwa kibiashara katika masoko mengi Afrika na hata soko la kimataifa huko Marekani na Ulaya. Kadri uwindaji wa nyama pori unavyozidi kuongezeka kutoka misituni hadi kwenye maeneo ya Savana, sehemu kubwa sana imekosa wanyama wakubwa hasa wanyama wenye kwato wa saizi ya kati hadi saizi kubwa kama vile nyumbu, punda milia, nyati na swala ambao ni chakula kikuu cha simba. Hata maeneo yanayolindwa makubwa yameathiriwa na uwindaji wa nyama pori, ikiwemo Serengeti ambapo maelfu kwa maelfu ya nyumbu huuawa kwa kutumia mitego kila mwaka.[4] Ukiachilia mbali kupungua kwa wanyama wa mawindo, mara nyingi simba hujikuta wamenasa na kuuawa kwenye mitego ya majangili waliyotega kwa ajili ya mawindo ya simba. Huko Msumbiji kwenye hifadhi ya Taifa ya Niassa, mitego ni tishio kubwa sana kwa simba, ikisababisha asilimia 52 ya vifo vyao.[5]

Vitisho vipya vinajitokeza, ikiwemo biashara inayoendelea kukua ya mifupa ya simba na sehemu nyingine za mwili. Mbali na matumizi ya bidhaa hizi kwenye tamaduni za Kiafrika kama vile sherehe na mila, simba pia wanauawa kama mbadala wa mifupa ya simba marara huko Asia.

Habari njema ni kwamba kuna suluhu kwa vitisho vingi dhidi ya simba. Sehemu yoyote ambapo shinikizo la kibinadamu lilipungua, uoto wa Savana, idadi ya wanyamapori wake hasa hasa simba ilirudi kama zamani. Labda hatua muhimu zaidi katika kupata uhakikisho wa maisha ya simba ni kufanya uhamasishaji mkubwa ili kupata msaada utakaowezesha ulinzi na usimamizi mzuri wa mfumo wa Maeneo Yanayolindwa (PAs). Uhifadhi wa simba wenye mafanikio unahitaji rasilimali nyingi zaidi ya zile zilizotengewa katika nchi zenye hifadhi. Nje na maeneo haya, migogoro inayosababishwa na simba kushambulia mifugo ni lazima ishughulikiwe. Kupunguza wepesi wa simba kushambulia mifugo pamoja na kuwahamasisha watu kutambua thamani ya simba ni hatua muhimu za kusonga mbele.

**Matumaini yapo kwa simba wa Afrika—vitisho vinajulikana, suluhu zipo na hamasa ya kidunia ya kuikomboa spishi hii adhimu inajidhihirisha—ila dunia ni lazima iungane pamoja kuhamasisha muitikio wake kama ilivyofanya mwaka mmoja uliopita ili kuleta mabadiliko ya kweli.**

# ATHARI YA CECIL

Kuna sababu nyingi kwa nini simulizi ya Cecil iligusa vyombo vya habari na jamii; kitendo cha kwamba alikuwa ni simba mwenye jina na alikuwa anajulikana sana kwa watafiti na watalii wa Hifadhi ya Taifa ya Hwange; na kwamba alikuwa amevishwa kola ya kielektroniki; na kwamba aliuawa kumfurahisha Mmarekani tajiri; kutanganwa kwa kifo chake kulikojaa majonzi na mtangazaji maarufu wa habari huko Marekani; kusambaa kwa haraka kwa picha zake na maoni yaliyotolewa kwenye mitandao ya kijamii. Japokuwa mwindaji hakuhukumiwa kwa uhalifu, vitu hivi vilipelekea dunia nzima kuingia kwenye harakati za kulipiza kifo chake.

Tangu siku hiyo taasisi mbalimbali za kiserikali, vikundi vya wanaharakati na taasisi za kisayansi zimechukua hatua. Baadhi ya mataifa ya Magharibi yaliongeza vizuizi vingi zaidi dhidi ya usafirishaji wa nyara za simba. Ufaransa na Uholanzi zimepiga marufuku uingizaji wa moja kwa moja wa nyara za simba, Uingereza imetoa onyo kali kwa tasnia ya uwindaji na kwa serikali katika nchi zinazoruhusu uwindaji wa simba kuboresha utendaji wao au la sivyo wapigwe marufuku kusafirisha nyara.[6,7] Australia ilipiga marufuku usafirishaji wa nyara mapema mwaka huu, kwa kile kinachosemekana kama muitikio dhidi ya uhamasishaji dhidi ya uwindaji wa simba wa kufugwa.[8] Mashirika makubwa ya ndege kama vile Delta, United na American Airlines, zimetangaza kuwa zitasitisha kusafirisha nyara za simba, chui, tembo, vifaru na nyati[9], na hivyo kuungana na British Airways pamoja na Virgin Atlantic, ambazo tayari zilishapiga marufuku usafirishaji wa nyara.[10]

Mnamo Januari mwaka 2016, kufuatia uchapishwaji wa utafiti wa kusikitisha unaoonyesha kuwa idadi kubwa zaidi ya simba wa Afrika inazidi kupungua Idara ya Marekani ya Uvuvi na Wanyamapori iliwapa simba wa Afrika Magharibi na Afrika ya Kati hadhi ya kuwa spishi iliyo hatarini kutoweka, na kwa simba wa Afrika Mashariki na Afrika Kusini hadhi ya hatarini kutoweka chini ya Kifungu cha Sheria cha Spishi zilizo hatarini kutoweka.[11]

Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi na Wanyamapori ya Marekani, Dan Ashe amesema kuwa kitendo hiki kitaongeza vizuizi kwa nyara za simba wa Kiafrika, kwa kumtaka mtu awe na nyaraka husika zinazoonyesha kuwa wamewinda katika hali inayohakikisha inawalinda wanyama. Vile vile, nchi zenye wanyama hawa zitatakiwa zionyeshe kuwa programu zao zinaboresha na kulinda idadi ya wanyamapori.[12] Hii inaonyesha mkakati madhubuti ambao aghalabu sana kuonekana pasi na jitihada nyingi pamoja na uthibitisho wa mara kwa mara. Harakati chache sana huweza kufikia vigezo hivyo.

Ni muhimu kutambua kuwa hata kabla ya kifo cha Cecil, baadhi ya nchi za Kiafrika zilishaanza kuchukua hatua, kwa kufuata makubaliano ya kisayansi kuwa uwindaji usiokua na usimamizi mzuri unaleta hasara. Katika miaka ya hivi karibuni, Msumbiji, Tanzania, Zambia na Zimbabwe zilianzisha mabadiliko makubwa juu ya uwindaji wa simba ikiwemo kupunguza idadi ya simba ambao watu wanaruhusiwa kuwinda. Kuna wakati, zote Zambia na Zimbabwe ziliwahi kuzuia uwindaji kwa kipindi cha miaka kadhaa ili kuwezesha idadi kuongezeka.

Pamoja na hatua chanya za nchi hizi pamoja na athari ya Cecil, bado hali ya simba wa Kiafrika ni mbaya.



Cecil akiwa Hifadhi ya Taifa ya Hwange, Zimbabwe. Paul Funston



"

**Mwaka mmoja uliopita, kutokana na kifocha Cecil, dunia nzima ilionyesha kusimama pamoja na Afrika katika kuokoa simba. Ila inasikitisha kuwa, tangu muda huo tumepoteza mamia kama si maelfu ya simba. Katika nchi nyingi spishi hii inazidi kuelekea pabaya. Ili kuwaokoa wanyama hawa adhimu, jamii ya kimataifa inahitaji kubadili hasira zao juu ya Cecil na kuielekeza katika utekelezaji na pesa za kusaidia serikali za Kiafrika, watu na taasisi zinazopambana kuokoa simba.**

**Dk. Luke Hunter**
**Rais, Panthera**


Burrard-Lucas.com

# IDADI YA SIMBA

Japokuwa hakuna makadirio sahihi ya kihistoria kuhusu idadi ya simba wa Kiafrika, ni dhahiri kuwa bara hili liliwahi kuwa makazi ya mamia kwa maelfu ya simba, waliotapakaa kila sehemu kasoro katika jangwa la Sahara na misitu ya ikweta kwenye bonde la Kongo. Ukoloni ulisababisha upungufu mkubwa, ambao umekuwa ukiendelea kadri idadi ya watu inavyozidi kukua.

Upungufu huu umezidi kuongezeka katika miaka ya hivi karibuni. Katika kipindi cha miongo miwili, idadi ya simba wa Kiafrika inaaminika kupungua kwa asilimia 43, huku simba 20,000 tu wakikadiriwa kubakia.[13] Ni nchi nne peke yake ndio zimekwenda tofauti na makadirio haya: Botswana, Namibia, Afrika Kusini na Zimbabwe.[14] Kwa pamoja, nchi hizi nne zinakadiriwa kuwa na asilimia 24-33 ya simba wa Kiafrika. Huku idadi ya simba imeongezeka kwa asilimia 12. Ila sehemu kubwa ya mafanikio haya ni kutokana na kuwaweka katika hifadhi za uzio zinazosimamiwa vyema na kuwezeshwa kifedha[15] — jambo ambalo haliwezi kufanywa kwa simba wengine waliobakia.

Mafanikio ya Afrika Kusini yanaficha kiwango cha upungufu kwingineko. Kwa mfano, idadi ya simba Afrika magharibi, Afrika ya Kati na Mashariki kwa pamoja zinakadiriwa kupungua kwa asilimia 60 katika kipindi hicho hicho.

Kwa sasa hivi Simba wanaishi katika asilimia 8 tu ya makazi yao ya asilia (ambayo yalikuwa na ukubwa wa kilomita za mraba Milioni 13) na inasemekana kuwa wameshatoweka kwenye nchi 12 za Kiafrika, huku kukiwa na uwezekano wa kupotea kwenye nchi nne zaidi.[16] Pia, mengi hayajulikani kuhusiana na simba wa Angola, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Somalia na Sudan Kusini ambapo vita za wenyewe kwa wenyewe pamoja na uwezeshaji au usimamizi mbovu wa Maeneo Yaliyohifadhiwa (PAs) unashukiwa kusababisha upungufu mkubwa.[17]

Simba wa Afrika wamewekwa na Jumuiya ya Kimataifa ya Uhifadhi wa Mazingira chini ya kundi la wanyama walio hatarini kwenye orodha yao ya spishi zilizo hatarini kutoweka.[18] Hata hivyo, simba wa Afrika Magharibi ndio wanaosemekana kuwa

hatarini zaidi kwani wamepoteza asilimia 99 ya makazi yao ya asili huku kukiwa na simba 400 tu (wakiwemo shiblina simba waliopevuka—simba chini ya 250 ni wale waliopevuka). Katika hawa 400, 300 wanatoka kwenye jamii moja ya W-Arly-Pendjari (WAP) wanaopatikana Benin, Burkina Faso na Niger.[19] Simba wa Afrika Magharibi, Afrika ya Kati na wale wa Asia wanafanana nasaba na inawezekana wakawa wanatoka kwenye spishi ndogo ***(Pantheraleoleo)*** tofauti na simba wa Afrika Mashariki na Afrika Kusini ***(Pantheraleomelanochaita).***

Nchi sita peke yake ndio zinazosemekana kuwa na simba pori zaidi ya 1,000: Tanzania na Kenya kwa Afrika Mashariki, na Botswana, Msumbiji, Afrika ya Kusini na Zimbabwe kwa Afrika ya Kusini. Nchi ya saba, Zambia inaweza kuwa na simba 1,000 au karibia na idadi hiyo. Idadi ndogo zaidi zinapatikana: Selous-Niassa (Tanzania/Msumbiji) Ruaha-Rungwa (Tanzania), Great Limpopo (Msumbiji / Afrika ya Kusini / Zimbabwe) Okavango-Chobe-Hwange (Botswana/ Zimbabwe) pamoja na Serengeti-Mara (Tanzania/Kenya).

Inasadikika kuwa kuna makao makuu kumi ya simba, makao haya yana angalau simba waliopevuka 500: Ruaha-Rungwa, Serengeti-Mara, Tsavo-Mkomazi (Kenya/ Tanzania), Selous (Tanzania), Luangwa (Zambia), Kgalagadi (Botswana, Afrika Kusini), Okavango-Hwange (Zimbabwe / Botswana), Mid-Zambezi (Msumbiji / Zambia / Zimbabwe), Niassa (Msumbiji), na Great Limpopo (Msumbiji, Afrika Kusini, Zimbabwe).



# THREATS

## VITISHO VIKUU




## AFRIKA MAGHARIBI




Vitisho Vikuu:

**1. Ujangili wa Nyama pori**
**2. Uvamizi wa Binadamu**

- Makazi Asilia
- Makazi ya Sasa
- Nje ya Makazi Asilia

Idadi Inayofuatiliwa: ↓ INAPUNGUA




## HALI YA SIMBA




**Simba ametoweka kabisa Afrika ya Kaskazini*

## AFRIKA MASHARIKI




Vitisho Vikuu:

**1. Migogoro ya Binadamu na Simba**
**2. Uvamizi wa Binadamu**

- Makazi Asilia
- Makazi ya Sasa
- Nje ya Makazi Asilia

Idadi Inayofuatiliwa: ↓ INAPUNGUA




## AFRIKA KASKAZINI




Vitisho Vikuu:


**1. Ujangili wa Nyama pori**
**2. Uvamizi wa Binadamu**

- Makazi Asilia
- Makazi ya Sasa
- Nje ya Makazi Asilia

Idadi Inayofuatiliwa: ↓ INAPUNGUA




## KUSINI MWA AFRIKA
### KASKAZINI MWA MTO ZAMBEZI




Vitisho Vikuu:

**1. Ujangili wa Nyama pori**
**2. Uvamizi wa Binadamu**

- Makazi Asilia
- Makazi ya Sasa
- Nje ya Makazi Asilia

Idadi Inayofuatiliwa: ↑ INAONGEZEKA *




*ukuaji kwenye idadi inayofuatiliwa ni ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Niassa, Msumbiji; kwingineko idadi ya simba inaweza kuwa inashuka kikanda

## KUSINI MWA AFRIKA
### KUSINI MWA MTO ZAMBEZI




Vitisho Vikuu:

**1. Migogoro ya Binadamu na Simba**
**Ujangili wa Nyama pori**

- Makazi Asilia
- Makazi ya Sasa

Idadi Inayofuatiliwa: ↑ IMARA / INAONGEZEKA




## MAELEZO JUU YA VIFO VYA SIMBA

Kwa sababu mauaji mengi ya simba ni kinyume na sheria na nadra kuripotiwa, makadirio ya idadi kamili ya simba waliouawa na watu haijulikani. Katika Hifadhi ya Taifa ya Niassa huko Msumbiji, uwindaji wa kitalii kwa mwaka 2014-2015 uliua simba 12, wakati angalau simba 42 waliuawa kinyume na sheria na wanajamii.* Hata hivyo makadirio yalifanywa katika eneo dogo lililokuwa likitanguliwa kwa karibu: vifo vingi zaidi vya simba havikurekodiwa. Pia uuaji kutokana na migogoro ni jambo dogo huko Niassa sababu wanajamii hawafugi ng'ombe—hii ni sababu kubwa ya vifo vya simba kwingineko. Kwa kuzingatia vipengele vyote, idadi ya simba waliouawa kinyume na sheria Africa ni mara tano zaidi ya simba waliouliwa kitalii na kwa baadhi ya maeneo inaweza kuwa hata mara 10 zaidi.

*Niassa Carnivore Project, HAIJACHAPISHWA

# KUPOTEA KWA MAZINGIRA ASILIA

Kuongezeka kwa idadi ya watu na wanyama Afrika katika kipindi cha miaka 25 na hivyo kupotea kwa makazi ya simba kutokana na kilimo ni moja ya sababu zilizosababisha kuzuka kwa vitisho vyote vikubwa dhidi ya simba. Simba wanapata shida kuishi na binadamu hasa wale ambao ni maskini na wanaoishi vijijini. Ukiachilia mbali kuwa moja ya sehemu ambazo zinakua kwa haraka katika idadi ya watu, Afrika pia ni sehemu yenye watu masikini zaidi wanaotegemea sana kwenye kilimo cha bustani.[20]

Baada ya kuwa wamepoteza theluthi tatu au zaidi ya makazi yao ya asili katika kipindi cha miaka 100, simba kwa sasa wanaishi katika Maeneo Yaliyohifadhiwa. Simba wanaishi katika asilimia 8 tu ya makazi yao ya asili.

Idadi ya watu Afrika inatarajiwa kuongezeka kwa kiasi kikubwa sana kutoka bilioni 1.2 hadi bilion 2.47 ifikapo mwaka 2050.[21] Nusu ya ukuaji huu umetabiriwa kutokea kwenye nchi 9 ikiwemo Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Ethiopia, Tanzania, na Uganda — zote zikiwa ni makazi ya simba.[22] Katika baadhi ya sehemu, idadi ya watu ni kubwa zaidi karibu na Maeneo Yaliyohifadhiwa[23] hivyo kuzidisha presha kwenye mfumo wa kiiokolojia ambao tayari umeshaelemewa.

Matumizi ya ardhi kwa ajili ya kilimo katika nchi za chini ya jangwa la Sahara yameongezeka kwa asilimia 25 baina ya mwaka 1970 na 2000, huku maeneo ya malisho kwa ajili ya wanyama wanaofugwa yakiwa yametanuka kwa asilimia 15 katika kipindi hicho hicho.[24]

"

**Idadi ya watu Afrika inatarajiwa kuongezeka kwa kiasi kikubwa sana kutoka bilioni 1.2 hadi bilion 2.47 ifikapo mwaka 2050.**

Upungufu mkubwa wa makazi ya wanyamapori umetokea katika nchi nyingi tu; kwa mfano mwaka 1990, ilikadiriwa kuwa wanyamapori wa Ivory Coast na Burkina Faso wamepoteza asilimia 79 na 80 ya makazi yao ya asili kutokana na kilimo.[25] Baina ya mwaka 2005 na 2050, maeneo ya ardhi ya kilimo katika nchi za chini ya jangwa la sahara yanategemewa kuongezeka kwa asilimia 21, huku mifugo ikitarajiwa kuongezeka kwa asilimia 73.[26]

## UVAMIZI WA BINADAMU NA MIFUGO KWENYE MAENEO YALIYOHIFADHIWA

Sasa hivi simba anaishi kwa kutegemea uhifadhi, huku idadi kubwa ya simba wakiishi ndani na pembezoni mwa Maeneo Yaliyohifadhiwa (PAs). Hifadhi za taifa, mapori ya akiba pamoja na maeneo mengine ya wanyamapori yanayolindwa ni muhimu kwa uhai wa spishi hawa. Japokuwa wanalindwa kwenye karatasi, hifadhi nyingi bado ziko dhaifu kwa vitisho vile vile vinavyojitokeza kwenye mazingira yanayokaliwa na watu nje ya mipaka yao. Kadri jinsi makazi ya binadamu katika uoto wa Savana yanavyozidi kukua, wakati mwingine vijiji huanzishwa pembezoni na ndani ya mipaka ya Maeneo yaliyohifadhiwa (PAs), na mifugo hulishwa pembezoni na mipaka; hii inapelekea katika migogoro isiyoepukika. Migogoro hii inachukua sura kuu mbili. Kwanza, mifugo inayokula kwenye Maeneo Yaliyohifadhiwa hushindana na mawindo ya simba jambo ambalo linaweza kupelekea kuharibika kwa uoto asilia na hivyo kusababisha kupungua kwa idadi ya wanyama asilia wala nyasi. Pili, ni rahisi kwa simba kukutana na mifugo ya nyumbani na huweza kupelekea mifugo kuuliwa. Jambo hili husababisha vifo vya visasi kutoka kwa wafugaji na wahifadhi pori. Uvamizi wa watu na mifugo yao kwenye Maeneo Yaliyohifadhiwa na shinikizo kwa simba sasa hivi inachukuliwa kuwa moja ya vitisho vitatu dhidi ya spishi hii katika Afrika Magharibi, Mashariki, Kati na Kusini.[27] Uvamizi wa binadamu pia unahusishwa na uwindaji haramu wa nyama pori—tishio lingine kubwa kwa simba na mawindo yao.



Mifugo iliyouawa na simba.



Nyumbu aliyeuliwa na mitego ya jangili. Save Valley Conservancy, Zimbabwe. T. Labat

# UJANGILI WA NYAMA PORI

Ulaji wa nyama pori—yaani nyama za wanyama wa porini—imekuwa ni sehemu ya tamaduni za Waafrika kwa miaka mingi sana. Zamani nyama pori ilikuwa inawindwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani katika jamii za vijijini, ila leo hii inauzwa kwenye masoko makubwa Afrika na hata kimataifa kwenye masoko yaliyopo Marekani na Ulaya (inakadiriwa kuwa tani 56 husafirishwa kila wiki kwenda Paris).[28] Kwa ngazi ya kitaifa, nyama pori ni chanzo nafuu cha protini kwa jamii zinazoishi vijijini. Kwa mfano Msumbiji vijijini, inagharimu dola za Kimarekani 3-4 kununua kuku na kiasi cha Dola za Kimarekani 1.60 kununua nyama pori kwa kiasi cha saizi ya kati.[29] Vile vile, walaji wenye uwezo kutoka mijini huona nyama pori kama kitoweo adimu na mara nyingi hugharimu zaidi ya asilimia 50 ya bei za kuku na samaki.[30]

Kuwinda ili kupata nyama pori kumekuwa ni tishio kubwa kwa wanyamapori kwa baadhi ya maeneo zikiwemo nchi kadhaa katika Afrika ya Mashariki na Afrika ya Kusini, ukiachilia mbali mataifa ya Afrika ya Kati na Afrika ya Magharibi ambapo kwa muda mrefu hili limekuwa ni moja ya changamoto za uhifadhi wanyamapori. Katika maeneo mengi ikiwemo PAs, biashara ya nyama pori imepelekea upungufu mkubwa wa idadi ya wanyama pori.

> “
>
> **Zamani nyama pori ilikuwa inawindwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, ila leo hii inauzwa kwenye masoko makubwa Afrika na hata kimataifa kwenye masoko yaliyopo Marekani na Ulaya.**

Kiasi kikubwa cha uwindaji wa nyama pori huwa ni haramu kwani mara nyingi wahalifu huwa hawana vibali, huwinda katika maeneo yaliyozuiwa kwa kutumia njia zilizoshakatazwa na huua wanyamapori bila kujali kama ni spishi inayolindwa au la, jinsia yao au umri.[31] Katika misitu ya Afrika ya Kati na Mashariki, nyama pori huchukuliwa kama sehemu muhimu katika usalama wa chakula na pia inatambuliwa kama chanzo muhimu cha protini kwa jamii za vijijini.[32] Hata hivyo uwindaji wa aina hiyo si endelevu na kukithiri kwake kumesababisha hali inayojulikana kama Kutoweka kwa Wanyama, ambayo imeleta athari kubwa sana kwa mnyama mwindaji wa msituni, Chui.[33]

Kwa hivi karibuni, uwindaji wa nyama pori umehamia kwenye eneo la uoto wa savana jambo ambalo limepelekea kutoweka kwa wanyama wakubwa.[34] Biashara ya nyama pori imeharibu uwezekano wa kupatikana ajira kutokana na utalii pamoja na kazi zinazohusiana na utalii na imeathiri usalama wa chakula kama chanzo cha kutegemewa cha protini (endapo kama itasimamiwa vizuri), kwani chanzo hiki cha chakula kinaweza kutoweka haraka sana iwapo hakutakuwa na usimamizi au uangalizi.[35] Lakini pia, jamii husika zinapoteza sehemu ya urithi wao wa kale kadri wanyamapori wanavyopotea.

Simba wanahitaji wanyama wenye kwato wa saizi ya kati hadi kubwa ili waweze kuishi; hawawezi kuishi kwenye mazingira yasiyokuwa na spishi kama vile nyumbu, punda milia, kudu, swala pala, na kuru.[36] Spishi hizi pia zinapendwa sana na majangili wa nyama pori kwa kutumia bunduki, mitego na mitego inayotumiwa kumkamata mnyama mguuni (gin traps). Mitego iliyo rahisi kupatikana ya waya ni moja ya njia haribifu zinazotumika. Ni rahisi kuitega na hunasa wanyama wengi ila huua bila kujali na pia huua spishi ambazo hazikulengwa kama vile simba na wanyama wengine wanaokula wanyama wenzao.[37] Majangili wanaweza kuwa hawakagui mara kwa mara mitego na pia huitelekeza mara baada ya mzoga mmoja au miwili kutolewa, hivyo kupelekea uharibifu mkubwa. Katika Hifadhi ya Save Valley ya Zimbabwe, angalau wanyama 1,410 waliuawa na kuachwa waozee kwenye mitego katika kipindi cha miaka 9.[38]

Uwindaji wa nyama pori ni chanzo kikubwa cha kupotea kwa mawindo katika maeneo makubwa ambayo yalikuwa makazi ya simba; idadi ya wanyamapori wanaokula mimea imepungua kwa asilimia 52 Afrika Mashariki na kwa asilimia 85 kwa Afrika magharibi katika kipindi cha miongo mitatu.[39] Matukio ya uwindaji haramu uko juu katika maeneo yaliyo karibu na makazi ya watu, mara nyingi kwenye mipaka ya maeneo yaliyohifadhiwa.[40] Baada ya kutokomeza idadi kubwa ya wanyamapori kwenye maeneo ya pembezoni, sasa majangili wameongeza kuwinda wanyamapori walio ndani ya Maeneo Yanayohifadhiwa PAs. Hata Maeneo Yaliyohifadhiwa ambayo ni makubwa sana yameathiriwa katika baadhi ya maeneo. Kwa mfano hata katika hifadhi maarufu ya Serengeti, mamia kwa maelfu ya nyumbu huuliwa na mitego ya majangili kila mwaka.[41]

Harufu ya mizoga katika mitego hiyo huvutia simba hivyo inakuwa rahisi kwao kujitega, ambapo hujikuta wanakabwa, wanavuja damu hadi kufa au hufa kwa kiu. Huko Msumbiji kwenye hifadhi ya taifa ya Niassa, mitego ndio tishio kubwa zaidi kwa simba, huku ikiwa inahusishwa na asilimia 52 ya vifo[42] (zaidi ya samba 40) kila mwaka kwenye hifadhi hiyo peke yake.[43]

Hifadhi mbalimbali kwenye maeneo ya Angola, Kameruni, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Ivory Coast, Gabon, Malawi, Msumbiji, Tanzania na Zimbabwe, pamoja na zinginezo, zimekumbwa na upungufu mkubwa wa ujazo, idadi ya simba au kutoweka kabisa kwa simba kutokana na uwindaji wa nyama pori. Huko Afrika Magharibi, katika tafiti 17 kati ya 21 zilizofanyika, kiwango cha chini cha ulinzi na uwindaji wa nyama pori usiokuwa na usimamizi uliojitokeza, umetajwa kuwa chanzo kikuu cha kutoweka kwa simba.[44]


Simba aliyejeruhiwa. EgilDroge/Zambian Carnivore Programme

## VITISHO VIPYA: UWINDAJI HARAMU WA SIMBA

Kiwango cha ujangili wa mifupa ya simba pamoja na sehemu nyingine za mwili hakijajulikana bado ingawa biashara hii inaonekana kuongezeka.[45] Bidhaa za simba zinatumiwa kwenye shughuli za kimila na pia kama dawa, mapambo na hirizi katika nchi nyingi za Kiafrika ikiwemo Somalia, Nigeria, Benin, Burkina Faso, Kenya, Senegal na Kameruni.[46] Uchunguzi mmoja uligundua matumizi ya simba katika dawa za kienyeji huko Nigeria ambapo mafuta yake, nyama, mifupa, meno, mapafu, ngozi, macho, moyo na ini vilitumika kutibu maradhi mbalimbali.[47] Serikali ya Kameruni iligundua biashara ya ngozi ya simba "Kama moja ya sababu ya kupungua kwa idadi ya simba katika Afrika Magharibi na Kati."[48]

Ukiachilia mbali mahitaji kwa ajili ya matumizi ya "kitamaduni", kuna uthibitisho kuwa simba wanawindwa kiharamu kwa ajili ya matumizi ya dawa za Kiasia. Japokuwa si mojawapo ya dawa za kitamaduni za Kichina, sasa hivi mifupa ya simba inasafirishwa kihalali kwenda China kama mbadala wa bidhaa za simba marara ambazo ni adimu na haramu kwa kuweka kwenye mvinyo dawa, potions na dawa lishe. Bidhaa za simba marara zimekuwa zikitumiwa tangu karne na karne, huku zikiaminiwa kumpa nguvu mtumiaji, kutibu jongo, kuvimba, kifafa na pia kama mkuyati.[49] Ila kadri jinsi idadi ya simba marara inavyozidi kupungua, viwiliwili kutoka kwa wanyama wengine wa jamii ya paka ikiwemo chui na simba, vimeingia kwenye soko kama mbadala. Mamlaka ya Umoja wa Mataifa wa Biashara ya Kimataifa ya Spishi Walio hatarini (CITES) umegundua "Kuongezeka kwa biashara ya kimataifa ya sehemu za mwili za simba kwa ajili ya matumizi ya dawa za kienyeji za Kiafrika na Kichina utaongezeka sana kama ilivyoongezeka kwa wanyama wengine wakubwa wenye jamii ya paka.[50] Kuna uthibitisho kuwa sehemu za miili ya simba kutoka Afrika Mashariki, Magharibi na Kusini zimeingia kwenye biashara haramu ya wanyamapori huko Asia.[51] Ujangili wa sehemu za miili za simba (aidha kwa ajili ya biashara ya ndani au ya kimataifa) inaonekana kuwa ni tatizo katika Afrika Magharibi na Kati na baadhi ya sehemu za Msumbiji na Tanzania.[52]

## KUKAMATWA KWA SEHEMU ZA SIMBA
2004-2014

| Nchi | Vilivyokamatwa | Bidhaa Zilizokamatwa |
|---|---|---|
| Cameroon | 1 | 6 |
| Egypt | 1 | 1 |
| Ethiopia | 1 | 4 |
| Ghana | 1 | 1 |
| Kenya | 3 | 37 |
| Mozambique | 2 | 2 |
| Namibia | 3 | 4 |
| Nigeria | 2 | 5 |
| Sudan | 0 | 0 |
| Somalia | 2 | 75 |
| Tanzania | 10 | 126 |
| South Africa | 38 | 96 |
| Zambia | 3 | 76 |
| Zimbabwe | 10 | 89 |

Idadi zinawakilisha idadi ya sehemu za mwili wa simba zilizokamatwa kutoka nchi hizi.
Data kutoka UNEP-WCMC





# MIGONGANO BAINA YA SIMBA-BINADAMU

Kwa Waafrika wengi wanaoishi vijijini am-bapo bado simba wanapatikana kuishi na spishi hii ni changamoto kubwa. Simba ni mnyama mkubwa na hatari alaye nyama ambaye analeta tishio la kweli kwa mifu-go, na wakati mwingine binadamu. Simba wa-nachukiwa sana kwa sababu ya kuua mi-fugo, ambayo ni chanzo kikuu cha utaji-ri kwa mamilioni ya wafugaji. Kutokana na hili, simba wanateswa sana katika maeneo ya wafugaji. Nje ya Maeneo Yaliyohifadhiwa, mauaji ya kisasi na yale ya watu kujihami yanachukuliwa kuwa moja ya vitisho vikuu dhidi ya simba.[53]

Simba wako hatarini kuuliwa katika mauaji ya visasi. Tofauti na spishi zingine zenye tahadhari kama chui na fisi, simba huwa na kawaida ya kulinda mzoga wao wa mfugo dhidi ya binadamu na hivyo huwa ni rahisi kuuliwa. Mara nyingi, kuonekana kwa nyayo za simba—bila kujalisha kama mfugo umeuliwa au la—kunatosha kuanza kumuwinda. Na kwa vile simba anapenda mizoga ni rahisi kunaswa au kupigwa risa-si wakati akiwa anakula mzoga. Japokuwa kuwalisha wanyama pori sumu kumepig-wa marufuku katika nchi nyingi Afrika, ni sheria isiyosimamiwa wala kuhukumiwa vizuri na imeonekana kuwa ngumu sana kuidhibiti. Upatikanaji wa kirahisi wa vi-uatilifu vyenye sumu kali vilivyo halali ime-pelekea kupatikana kwa silaha nzuri ya kuua simba. Wakulima na wafugaji hunyunyizia sumu kama vile carbofuran kwenye mzoga ili ku-wavutia wanyama wanaowinda, kiten-do kin-achopelekea kuuliwa kwa simba, na spishi zingine zitakazokula mzoga, wakiwe-mo tai, chui, fisi na mbwa mwitu.[54] Katika baadhi ya maeneo, majangili wa pembe za ndovu, huweka sumu kwenye mabwawa ya maji ili kuua tembo, na kwa namna hiyo huua kila mnyama anayekunywa hayo maji akiwemo simba.

Athari za vifo vya mifugo kutokana na mashambulizi ya simba zinatofautia-na. Kifo cha mfugo mmoja kwa mfugaji mwenye mifugo michache yaweza kuwa jambo la kusikitisha sana. Watafiti wa-na-kadiria kuwa kila simba anayeishi pem-be-zoni mwa Hifadhi ya Taifa ya Tsavo East anawagharimu wafugaji kiasi cha Dola za Kimarekani 290 kwa mwaka kutokana na vifo vya mifugo.[55] Katika maeneo mengine simba huua ng'ombe wachache zaidi ukil-inganisha na mifugo mingine isiyo ya tha-mani: katika maeneo yaliyo mkabala na Hifadhi ya Taifa ya Waza huko Kameruni, simba walihusika kwa asilimia 3.1 ya vifo vya mifugo lakini walikadiriwa kuhusika na asilimia 22 ya hasara za kiuchumi—kama Dola za Kimarekani $370 kwa kila mmiliki.[56]

Athari za kisaikolojia ikiwemo hisia za chu-ki, nazo ni kubwa: watu wengi wanaoishi karibu na simba wana mtazamo hasi kuhu-siana na wanyama hawa, wanawaona kama vile wanyama waharibifu wanaotakiwa watokomezwe.[57] Katika baadhi ya matukio, wafugaji huwawinda kiharamu wanyama pori kama malalamiko kutokana na hasara zilizosababishwa kutokana na uwindaji na vyanzo vingine vya migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

Kwa vile uuaji wa simba unaofanywa na wananchi ni kinyume na sheria, makadirio ya kuaminika ya kiwango na athari yanako-sekana. Simba wa Hifadhi ya Taifa ya Nai-robi na wale wanaopatikana kwenye bonde la Kitengela, kidogo watokomezwe kabisa kutokana na kupigwa mikuki na watu am-bapo angalau simba 87 walikufa kati ya mwaka 1998 na 2005.[58] Kati ya mwaka 2001 hadi 2006,[59] angalau simba 108 na labda wengi zaidi ya hapo waliuawa katika eneo la kiikolojia la Tsavo-Amboseli (lililo-po baina ya Hifadhi za taifa za Amboseli na Tsavo West) huko Kenya. Huko Tanzania, zaidi ya simba 125 waliuliwa kati ya mwaka 2000 na mwaka 2005 katika eneo la kiiko-lojia la Tarangire-Manyara, na watu waliua angalau simba 35 katika Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro baina ya mwaka 1998 na 2004.[60]


Mpiga picha hajulikani

# UWINDAJI WA KITALII

Licha ya uwindaji wa kitalii kupewa ki-pa-umbele baada ya kifo cha Cecil, ni kitu kidogo ambacho kinachangia kupungua kwa idadi ya simba. Katika maeneo men-gi ambayo simba mwitu wanawindwa, pia wanakutana na vitisho vya uwindaji wa nyama pori pamoja na migongano na binadamu. Kwa pamoja, sababu hizi zinachangia kwa kiasi kikubwa sana ku-pun-guza idadi ya simba, Kuwinda kun-aweza kukawa tishio la ziada dhidi ya idadi ya simba ambao tayari wanapata shinikizo kubwa kutoka kwa binadamu.

Tofauti na spishi nyingi zilizo na kwato, ambao wameweza kubadilika simba wako hatarini kuwindwa kupitiliza kiasi: kuto-ku-wepo kwa madume kunaleta mvuruga-no ndani ya jamii ya simba; kunapelekea mauaji ya shibli wa simba; kunapunguza kiwango cha kuzaliana na kuishi; na ku-sa-babisha simba waliosambaratika ku-hamia katika maeneo hatarishi zaidi.

Nchi nane zina mazoea ya kusafirisha nyara za simba: Zimbabwe, Tanzania, Af-ri-ka Kusini, Botswana, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Msumbiji, Namibia na Zambia. Ila tuz-ipe sifa nchi hizi, katika miaka ya hivi kari-buni Msumbiji, Tanzania, Zambia na Zim-babwe zimefanya mabadiliko kuhusiana na uwindaji wa simba kwa kupunguza idadi ya simba watakaowindwa na kuongeza umri kwa nyara za simba dume zitakazowindwa. Kwa kutambua kuwa uwindaji wa kitalii un-asababisha kupungua kwa idadi ya simba, zote Zambia na Zimbabwe zimesitisha kwa muda uwindaji wa simba kwa ngazi ya ki-taifa na kimkoa ili kuruhu-su idadi ya simba iongezeke. Uongezekaji wa haraka wa sim-ba wakati wa usitishwaji huu ulionyesha kuwa uwindaji uliokithiri unapunguza idadi ya simba pori.

> “
> **Kama kifo cha Cecil kilivyoonyesha kuwa uwindaji ni mgumu kuzuia na ni ngumu pia kuhakikisha kuwa unakuwa endelevu kikweli kweli.**
>
> ***- Peter Knights, Mkurugenzi Mtendaji wa WildAid***

Utafiti wa hivi karibuni umeonyesha jin-si gani ilivyokuwa ngumu kupata fom-yula sahihi. Katika eneo la utafiti kati ya hifadhi ya taifa na eneo la kuwinda lililo mkabala na hifadhi hiyo kwenye Bonde la Luangwa huko Zambia, uwindaji unaun-gana pamo-ja na vifo vingine vinavyosa-babishwa na binadamu ikiwemo mauaji ya kisasi yan-ayofanywa na wafugaji pamoja na mitego.[61] Mbinu ya utafiti ya kisasa ilionyesha kuwa, mpaka aina nyingine za mauaji zitakapopungua kwa kiasi kikub-wa, uwindaji wa aina yoyote ule ni lazima utachangia upungufu mkubwa wa idadi ya simba katika kipindi cha miaka 25.

Jinsi sayansi inavyozidi kuonyesha athari hasi za uwindaji wa kitalii wa simba na wanyama wengine wenye kiwango kido-go cha vifo, ni lazima vizuizi vya uwindaji vi-ongezwe. Hata hivyo changamoto kub-wa kwa wapinzani wa uwindaji ni namna ya kuwa na vyanzo mbadala vya fedha kwa serikali, wamiliki wa ardhi na jamii ili ku-unga mkono usimamizi wa wanya-mapori, endapo utasitishwa

# UWINDAJI WA KITALII: JE UNASAIDIA AU KUDHURU UHIFADHI WA WANYAMA PORI?

## WATETEZI WANASEMA HIVI:

- Inachangia kwa kiasi fulani katika gharama za uendeshaji za mamlaka za hifadhi za taifa katika baadhi ya nchi.
- Inasaidia kupatikana kwa mapato kutokana na maeneo makubwa ya taifa kwa ajili ya wanyamapori ikiwemo Hifadhi za taifa kupitia mapori ya akiba na mapori tengefu.
- Inanufaisha wanyamapori walio katika ardhi ya jamii au ya mtu binafsi.
- Inafanya jamii zikubali kuishi pamoja na wanyamapori endapo manufaa ya uwindaji yatatumika katika jamii husika.
- Katika baadhi ya maeneo, wawindaji huchangia katika jitihada za kuzuia ujangili na uwepo wa wawindaji utasaidia kupunguza ujangili, uvamizi wa binadamu na vitisho vingine.
- Unalenga kuwinda simba ambao wameshaacha kuzalisha hivyo haiathiri idadi yao.
- Uwindaji unaweza kufanyika kwenye mazingira yenye miundo mbinu mibovu, au yasiyovutia au hata kwenye sehemu zilizo na migogoro ya kisiasa ambapo utalii wa kawaida hauwezekani

## WAPINZANI WANASEMA HIVI:

- Mara nyingi hulenga kuwinda madume ambayo bado yanazalisha ili waweze kupata nyara nzuri zaidi.
- Kuua madume mengi kunaweza kusababisha mauaji ya shibli na kupungua kwa uzalishaji, hivyo kupungua kwa idadi.
- Mara nyingi ni chanzo cha vifo kutokana na sababu nyingine za kibinadamu kama vile kutega mitego na kuua kwa kisasi.
- Inaweza kupelekea idara za serikali kutegemea pesa za uwindaji, na hivyo kuongeza idadi ya simba wanaoweza kuuliwa.
- Mara nyingi hufanyika mipakani mwa hifadhi za taifa hivyo kuua simba walio kwenye Maeneo Yaliyohifadhiwa.
- Mara nyingi uwindaji hauleti pesa za kutosha kuendesha na kusimamia vizuri maeneo.
- Mara nyingi hushindwa kugawa mapato sawa baina ya jamii, na idara za serikali zinaweza kuwa wazito kugawa majukumu kwa wanajamii kwa sababu bajeti kuu zao zinategemea mapato yanayotokana na uwindaji.
- Kanuni za uendeshwaji zinakiukwa sana na ni ngumu kudhibiti (kama ilivyo kwa mfano wa Cecil).
- Mara nyingi hainufaishi walengwa kwani rushwa inazuia mapato kuwafikia walio vijijini au mtu mmoja mmoja.

## SIMBA WA KUFUGWA NA UWINDAJI WA SIMBA WANAOFUGWA

Kiasi cha simba 1,000 wa kufugwa wanauliwa kihalali kila mwaka katika kile kinachoitwa "Uwindaji wa simba wanaofugwa" huko Afrika Kusini,[62] utaratibu ambao unagharimu chini ya theluthi moja ya gharama za kawaida za uwindaji (Dola za Kimarekani 20,000 badala ya 76,0000).[63] Katika uwindaji huu, mwindaji aliyelipa anamuua simba aliyefugwa katika eneo lililozungushiwa, hivyo anajihakikishia safari fupi na nyara bora. Uwindaji wa simba wa kufugwa wa Afrika Kusini unalisha kihalali biashara ya sehemu za mwili za simba, hasa hasa mifupa yake, kwenda bara la Asia kama mbadala wa bidhaa haramu za simba marara katika mvinyo dawa, dawa za majimaji, na dawa lishe. Kwa ujumla, mifupa 1,160 ya simba ilisafirishwa kihalali kutoka Afrika Kusini kati ya mwaka 2008 na 2011.[64] Maeneo mengi ya kuzalisha simba Afrika Kusini yanapata faida maradufu kwa kutoa huduma ya kulisha shibli wa simba na kuwa karibu na simba jambo ambalo linawavutia watalii wengi na watu wanaojitolea. Watoto wa simba hutenganishwa na mama zao muda mfupi baada ya kuzaliwa na hupewa maziwa ya chupa, ili simba jike awe tayari kushika mimba tena.[65] Shibli wakishakuwa wakubwa, wengi wao huuzwa kwenye ranchi za kuwinda na wazalishaji wa simba kwa ajili ya soko la uwindaji wa simba wa kufugwa.

Watetezi wa uzalishaji simba na uwindaji wa simba wa kufugwa wanadai kuwa wanapunguza presha kwa simba mwitu kwa kutosheleza utashi wa wawindaji na mifupa ya simba kutoka kwa simba aliyefugwa. Ila hakuna uthibitisho wa madai hayo. Kwani kwa kiasi kikubwa wawindaji wa simba wa kufugwa ni watu tofauti na wawindaji wa kawaida, na kuongezeka kwa simba wanaofugwa hakujasaidia sana kupunguza uhitaji wa uwindaji wa simba pori. Wakati huo huo biashara ya Afrika Kusini ya mifupa imetengeneza fursa halali ya biashara ya mifupa ya simba jambo ambalo halikuwa likifanyika Asia. Kwa sababu kuna baadhi ya walaji wanaoamini kuwa mifupa ya simba pori ndio inayofaa zaidi kuliko ya simba wanaofugwa, ni dhahiri kuwa sehemu za mwili za simba waliouliwa kiharamu zitaingia kwenye masoko hayo hayo.


Shibli katika shamba la uzalishaji. Pippa Hankinson

# SULUHU

Hatima ya simba wa Afrika haieleweki. Ingawa kuna kiasi cha simba ambao watakuwa salama kwa muda mrefu, wengi zaidi wako kwenye shinikizo na bila kuwepo kwa jitihada za makusudi basi watatoweka. Afrika bado ina maeneo makubwa ya mapori. Kwa bahati nzuri misitu ya savana ambayo simba huhitaji inavumilia. Kokote pale ambapo shinikizo la kibinadamu lilipungua, uoto huu, idadi ya wanyamapori wake na hasa simba ilirudi kama zamani. Suluhu zipo na wala si ngumu ila zinahitaji mwitikio wa kidunia.

## KUIMARISHA MAENEO YALIYOHIFADHIWA

Yawezekana kuwa hatua muhimu zaidi katika kuhakikisha maisha ya simba wa Afrika ni kufanya uraghbishaji mkubwa wa uwezeshaji wa Maeneo Yaliyohifadhiwa ya bara hili. Kama yakilindwa, maeneo yatahakikisha uhai wa muda mrefu wa simba na spishi nyingine. Maeneo Yaliyohifadhiwa ya Afrika yanajumuisha kilomita za mraba milioni 1.51 ya makazi ya simba—eneo lenye ukubwa mara mbili zaidi ya Texas. Hata hivyo, nyingi hazina uwezeshwaji wa kutosha na asilimia 31 tu ya Maeneo Yaliyohifadhiwa yenye simba yanayolinda spishi hii kwa asilimia 50 au zaidi ya natural density kama tu wangekuwa wanakufa kwa kawaida.[66]

Kuimarisha maeneo yaliyohifadhiwa ni fursa kubwa ya kuhifadhi wanyamapori ambayo inahitaji msaada mkubwa. Kulingana na gharama za uendeshaji za NGO African Parks, katika hifadhi saba kutoka nchi sita ambazo shirika hili linasimamia, usimamizi mzuri wa Maeneo Yaliyohifadhiwa yote yenye simba yatahitaji bajeti ya mwaka ya angalau Dola za Kimarekani Bilioni 1.25 ($830 ± $285/kilomita za mraba/mwaka, zilizothaminishwa kwa viwango vya mwaka 2015).[67] Kikao cha Cecil ambacho kitaendeshwa na WildCru pamoja na Panthera Septemba 2016, kitataka kufahamu kiasi kilichopelea kama sehemu ya shabaha za jitihada za kidunia.

Kwa nini hii inahitaji uwekezaji mkubwa? Kwa mfano, utekelezaji wa sheria za kuzuia ujangili ni gharama na una changamoto. Vivyo hivyo ushiriki mzuri na jamii na hatua za kushughulikia migogoro ya wanyamapori, zinahitaji rasilimali watu na rasilimali fedha za kutosha. Wasimamizi wa Maeneo Yaliyohifadhiwa wanahitaji wafanyakazi wa kutosha ili kufanya doria na kutekeleza masuala ya kiofisi. Mashine zinahitajika ili kufanya marekebisho ya barabara na miundo mbinu, magari na mafuta pia yanahitajika kwa ajili ya doria. Msaada wa kianga nao ni njia muhimu sana ya kugundua na kuchukua hatua dhidi ya uwindaji haramu. Ingawa pesa zinaweza kupungua endapo jamii itashirikishwa kikamilifu kwenye jitihada za uhifadhi, rasilimali za kutosha zinaendelea kuwa na umuhimu, kwa sababu kiwango fulani cha uwindaji haramu hufanyika mbali na mipaka ya Maeneo Yaliyohifadhiwa.

> “
>
> **Wakati matokeo ya uhifadhi yakiendelea kupatikana, kuimarisha msaada katika Maeneo yaliyohifadhiwa kutatengeneza ajira, kutavutia zaidi utalii na kuchochea ukuaji wa uchumi.**

Wakati matokeo ya uhifadhi yakiendelea kupatikana, kuimarisha msaada katika Maeneo yaliyohifadhiwa kutatengeneza ajira, kutavutia zaidi utalii na kutachochea ukuaji wa uchumi. Matokeo haya yatapatikana vizuri kupitia ubia baina ya sekta binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali na mamlaka za kitaifa za uhifadhi wa wanyamapori, jambo ambalo litasaidia kupatikana kwa uwezeshaji wa muda mrefu wa kifedha pamoja na msaada wa kiufundi.

### HATUA ZA KUCHUKUA

- ***Kufanya uraghbishaji wa haraka ili kuongeza msaada katika usimamizi wa Maeneo Yaliyohifadhiwa ya Afrika; msaada ni lazima utoke kwenye serikali za Kiafrika pamoja na jumuiya ya kimataifa. Msaada kama huo utaimarisha uhifadhi wa simba na kusaidia kuchochea maendeleo katika sekta ya utalii, ukuaji wa uchumi na kutengeneza ajira.***
- ***Kuimarika kwa mahusiano zaidi baina ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na sekta binafsi pamoja na mamlaka za kitaifa za kuhifadhi wanyamapori kwa ajili ya usimamizi wa Maeneo Yaliyohifadhiwa yasiyokuwa na fedha za kutosha. Utaratibu kama huu unasaidia jitihada za mamlaka za kitaifa za kuhifadhi wanyamapori kwa kuipatia msaada wa kifedha wa muda mrefu pamoja na msaada wa kiufundi.***
- ***Kuhakikisha kuwa wanajamii wanapata vyakula vyenye protini bila kuhitaji kuwinda nyama pori kupitia kuongeza uwezo wa wanajamii kufuga mifugo; kuwawezesha kupata chanjo za mifugo za bei nafuu na matibabu ya afya ili kupunguza magonjwa, na kutumia afua za kupunguza hasara zinazosababishwa na wanyama wala nyama.***


Cecil, Zimbabwe. Craig Taylor

## FAIDA NA HASARA ZA KUWEKA UZIO

Katika baadhi ya maeneo ya Afrika, hasa hasa Afrika Kusini, Maeneo Yaliyohifadhiwa huzungushiwa uzio aidha kiasi au sehemu yote. Uzio unasaidia kuzuia uvamizi wa watu na mifugo kwenye hifadhi, na husaidia kupunguza migogoro inayotokana na wanyamapori hatari kuhamia kwenye vijiji vya karibu. Kuweka uzio kumesaidia baadhi ya hifadhi, hasa zile zilizo chini ya upana wa kilomita za mraba 1,000 kuwalinda simba.[68] Hata hivyo uwekaji wa uzio una hasara zake ikiwemo utenganishwaji wa ikolojia, kuharibu njia za wanyama kuhama, kutengwa kwa spishi za wanyama na matumizi ya vifaa vya kutengenea uzio katika ujangili wa kutumia waya.[69]

# KUSHUGHULIKIA MIGOGORO BAINA YA SIMBA NA WATU

Popote pale palipo na watu pamoja na mifugo yao, simba hawawezi kuishi mpaka hapo chanzo kikuu cha mgogoro—uharibifu unaofanywa na simba—utakapotambuliwa. Huu ni mchakato muhimu sana katika hifadhi zilizopo nje ya maeneo yanayohifadhiwa, ardhi iliyo pembezoni mwa Maeneo Yaliyohifadhiwa na ndani ya maeneo haya ambapo watu huwalisha machunga wanyama wao kinyume na sheria.

Kipaumbele cha kwanza ni kupunguza udhaifu wa mifugo. Ingawa vifo vinavyosababishwa na simba pamoja na wanyama wengine wala nyama vinaweza vikawa ni jambo la kawaida katika maeneo yenye makazi ya binadamu Afrika, vinaweza kupunguzwa ili malalamiko dhidi ya simba yapungue. Miradi iliyofanikiwa ilifanya kazi na wanajamii kujenga mabanda salama ya usiku na kuboresha nyanja nyingine za ufugaji. Kikawaida wanajamii wanaajiriwa ili kutoa tahadhari pale simba wanapokaribia katika maeneo yenye mifugo, kuwapa pole wale waliopoteza mifugo yao na kuwashauri wasilipize kisasi.

Ukiachilia mbali kupunguza vifo vinavyosababishwa na simba, watu pia wanahitaji kuthamini uwepo wao. Utalii ni moja ya njia muhimu za kuiingizia jamii mapato, na kuwapa simba thamani kama moja ya spishi inayotafutwa sana duniani. Lakini hata hivyo, kama ulivyo uwindaji, mara nyingi utalii umeshindwa kuzipa jamii husika manufaa ya kubeba mzigo mzito wa kuishi na simba na si mara zote njia hii huwa inafaa hasa kwenye maeneo yaliyo mbali sana au yaliyokuwa nyuma kimaendeleo. Kuna haja ya njia mpya, za kibunifu na zitakazokubalika kote za kuingiza kipato ili kuwahamasisha Waafrika kuishi na simba.

> **Ingawa vifo vinavyosababishwa na simba pamoja na wanyama wengine wala nyama vinaweza vikawa ni jambo la kawaida katika maeneo yenye makazi ya binadamu Afrika, vinaweza kupunguzwa ili malalamiko dhidi ya simba yapungue.**

## HATUA ZA KUCHUKUA

- ***Kutambua vyanzo bunifu vya fedha ili kusaidia ulipaji wa fidia, ambapo jamii zinanufaika moja kwa moja kwa kulinda na kuishi na wanyamapori (bila kutegemea mapato kutoka kwenye utalii au uwindaji). Ulipaji huu unaweza ukawa kwa mfumo wa fursa za elimu zilizoboreshwa au huduma bora zaidi za kiafya, hivyo kutengeneza jukwaa linaloambatanisha uhifadhi pamoja na malengo ya kimaendeleo.***
- ***Kubuni miradi ya maendeleo ambapo jamii zitashiriki katika kupunguza uharibu wa simba kwa mifugo kupitia maboresho makubwa ya mbinu za ufugaji—kama vile kuhamasisha ufungwaji wa wanyama wakati wa usiku, kuwa na wanyama wakati wanaenda kwenye malisho na kuhakikisha kuwa wanyama hawaachwi malishoni nyakati za usiku.***
- ***Kubadili viuatilifu vyenye kuua wadudu wengi ambavyo ni sumu kwa wanyamapori na kutumia viuatilifu ambavyo vinaua wadudu husika na ambavyo si hatari kwa wanyamapori.***


Christian Sperka


## FIDIA DHIDI YA MANUFAA

Kuwapa fidia wafugaji ambao mifugo yao iliuliwa na simba yaweza kuonekana kama ni suluhu iliyo dhahiri, na baadhi ya wadau huko Kenya wameitumia njia hii kwa mafanikio katika kupunguza mauaji yanayofanywa na simba. Ni mbinu nzuri kutumia hasa wakati wa migogoro kama vile baa la njaa ambapo matukio ya simba kuua mifugo huongezeka. Hata hivyo, baadhi ya programu zilizofanikiwa nazo zimeona makali ya mauaji yanayofanywa na simba. Mara nyingi ulipaji wa fidia huwa hausaidii kupunguza uharibifu wa mifugo na unaweza kuchangia katika mbinu mbovu za ufugaji wa kuondosha umuhimu wa kuilinda vyema mifugo dhidi ya simba. Ulipaji wa fidia utakuwa unatoa thamani ya moja kwa moja ya kifedha ya simba: Watu watakuwa wanalipwa kulingana na idadi ya simba waliopo katika eneo lao na uthibitisho wa kuzaliana kwao kunaongeza gharama. Japokuwa bado ipo majaribuni, malipo haya yana umuhimu mkubwa.

## JE KUPUNGUZA MIGOGORO KUNASAIDIA?

Kaskazini ya Namibia, jitihada za pamoja baina ya shirika lisilo la kiserikali la Kwando Carnivore Project, na Panthera ina lengo la kupunguza mauaji ya kisasi dhidi ya simba yanayofanywa na wafugaji wanaoishi katika maeneo tete karibu na Maeneo Yaliyohifadhiwa. Kwa ushirikiano wa wanajamii, mradi umejenga mabanda makubwa na yaliyo salama ili kuipa mifugo sehemu salama ya kukaa wakati wa usiku. Mabanda haya yanazuia uwezo wa simba kuwachukua kwa urahisi mifugo kutoka katika makazi yao ya usiku, jambo ambalo zamani lilikuwa la kawaida mno katika mabanda lege lege yaliyokuwa yanatengenezwa kwa miti ya Acacia. Mabanda mapya pia yanaweza kuhimili mkusanyiko wa ng’ombe wenye uoga pindi watakapokuwa wamenusa harufu ya simba. Tangu kuanza kwa mradi huu, mauaji ya mifugo nyakati za usiku yamekwisha kabisa, (japokuwa mifugo bado inaweza kuliwa na simba endapo haitachungwa vizuri wakati wa malisho mchana). Katika kipindi hicho hicho idadi ya simba waliouliwa na watu imepungua kutoka 20 kwa mwaka 2013, kabla mabanda salama hayajajengwa hadi mmoja kwa mwaka 2015 hadi kufikia vifo sifuri kwa mwaka 2016.


Christian Sperka


Christian Sperka

# MABADILIKO KATIKA UWINDAJI WA KITALII WA SIMBA

Kuna makubaliano makubwa baina ya wanasayansi wa masuala ya simba kuwa kama uwindaji wa kitalii utaendelea, lazima kuwe na mabadiliko ya haraka na yenye wigo mpana kuhusiana na hili suala. Ukizingatia changamoto zilizopo katika kushughulikia aina nyingine za vifo vya simba, uwindaji endelevu utakuwa mgumu kutekelezeka katika maeneo mengi. Machapisho mengi ya siku za hivi karibuni yametoa mwongozo wa kisayansi juu ya baadhi ya mabadiliko muhimu ili kupunguza hatari zinazohusiana na uwindaji wa simba.[70, 71]

## HATUA ZA KUCHUKUA

- ***Kuhakikisha kuwa kuna vizuizi vikali vya umri katika kila nchi ambapo simba anawindwa na inabidi waongeze umri unaoruhusiwa kuwa miaka 7.***
- ***Kunyambulisha mfumo mpya wa kugawa idadi ya simba watakaowindwa kulingana na umri wa simba waliowindwa mwaka jana, ambapo idadi itapunguzwa kama simba wadogo watakuwa waliwindwa.***
- ***Kuhakikisha kuwa kuna ukaguzi unaojitegemea wa umri wa simba watakaowindwa, na kwamba michakato ya umri pamoja na ugawaji wa idadi inakuwa wazi.***
- ***Katika maeneo yote kasoro yale yanayosimamiwa vizuri, zuia uwindaji kwa Kilomita za mraba 0.5/1,000.***
- ***Katika mahali ambapo idadi ya simba imewindwa kupitiliza kiasi na imeathiriwa kwa kiasi kikubwa na uwindaji, pasitishwe kwa muda ili kuwapa nafasi idadi iongezeke na wafikirie kuanza tena uwindaji endapo kutakuwa na mabadiliko.***
- ***Kufanya mabadiliko ya michakato ya ugawaji wa vitalu vya kuwinda kwa kuondosha rushwa na kuhakikisha kuwa wawindaji waaminifu tu ndio wanaopewa maeneo.***
- ***Kutoa muda mrefu wa uwindaji, kukiwa na majukumu yanayoeleweka ya kuzuia ujangili na kazi za kijamii watakayopangiwa wawindaji.***
- ***Kufanya mapitio ya mara kwa mara ya utendaji wa wawindaji kupitia concession management.***
- ***Kutambulisha utoaji wa cheti kiasi kwamba wawindaji watakaopata nyota ya dhahabu ya kuwa na rekodi nzuri ya uwindaji endelevu, uhifadhi na kazi za kijamii watakuwa wakitambuliwa kwa urahisi na wateja.***
- ***Kuzuia uwindaji wa simba wa kufugwa huku kukiwa na udhibiti mkali wa uwindaji wa simba pori na kuhakikisha bei ya uwindaji wa simba pori ni kubwa.***

# KUPUNGUZA MAHITAJI YA VIUNGO VYA SIMBA

Ili kuhakikisha Simba wa Afrika hawapati hatma kama ya Simba marara wa Asia, kampeni za elimu katika mabara yote, Afrika na Asia, na hususani China, zinahitajika ili kushughulikia uhitaji wa viungo vya simba. Mamlaka za UN CITES tayari imeona biashara ya kimataifa ya viungo vya samba ina uwezekano wa kuongezeka bila udhibiti, kama ilivyokuwa kwa wanyama wengine wakubwa jamii ya paka. Suluhisho la sasa ni kuzima uhitaji kabla madhara zaidi kutokea-na inawezekana kuangamiza-Simba pori wa Afrika. Kampuni zinahitajika kuwaelimisha watumiaji na wanaoweza kuwa watumiaji kuhusu hali iliyopo ya simba, na kuwavunja moyo kutumia mifupa, ngozi na viungo vingine kwa ajili ya dawa za kitamaduni kwa kuondoa imani hizi potofu za kitabibu, na kuhamasisha uungaji mkono wa jitihada za utunzaji urithi wa asili wa Afrika.



Simba Jike Nairobi National Park, karibu na mji mkuu ulio na pilika pilika. Peter Knights

# MITAZAMO KUTOKA NCHI ZA KIAFRIKA[72]

Wajumbe kutoka nchi 28 za Afrika zenye hifadhi za simba walikutana nchini Uganda kuanzia tarehe 30-31 Mei, 2016 kujadiliana kuhusu uhifadhi, usimamizi na urejeshaji wa simba na makao yake barani Afrika. Makubaliano yafuatayo yalifikiwa:[72]

- Walikubaliana kuwa kuna uhitaji wa kuboresha ukusanywaji wa taarifa za kisayansi na data za idadi ya simba pamoja na kuangalia mabadiliko ya idadi.

- Walizitaka nchi zenye hifadhi kuimarisha sheria kuhusu uhifadhi wa simba na kuhamasisha utaratibu sahihi wa matumizi ya ardhi, kuanzisha miundo muafaka ya utawala na kuboresha hatua za kisheria kuhusiana na wafugaji wa ng'ombe na majangili

- Zilisisitiza mahitaji ya maendeleo ya mikakati ya kitaifa na mbinu sahihi za kusimamia uhifadhi wa simba katika ngazi ya kitaifa

- Walikubaliana usimamizi wa maliasili unaofanywa na jamii, kutoa faida kwa jamii zinazoshiriki kwenye uhifadhi wa simba, kugawana manufaa na uanzishwaji wa hatua za kupunguza madhara yataongeza idadi ya simba na ni muhimu kwa uhifadhi wa simba

- Wameitisha uanzishwaji wa mfumo mzuri wa kiikolojia na matumizi ya ardhi yanayojali wanyamapori, kuhakikisha shughuli za kilimo na za uchimbaji madini hazizuii uhifadhi wa simba



- Uliangazia jinsi mchango wa uwindaji wa kitalii unavyosaidia uhifadhi wa simba katika baadhi ya nchi, ambapo unafanywa kwa kutumia idadi zilizopatikana kisayansi, kwa kuzingatia hadhi, umri na jinsi ya mnyama

- Uliangazia athari mbaya zinazoweza kujitokeza kutokana na kupiga marufuku usafirishaji kwenda nje wa nyara za simba kwa idadi ya sasa ya simba

- Kutambua uhitaji wa ushirikiano katika mipaka ya mfumo wa usimamizi kutokana na idadi kubwa ya simba wanaohama kutoka mpaka mmoja kwenda mwingine

- Zimeitaka CITES, CMS na IUCN kutoa taarifa za kisayansi ili zisaidie uanzishwaji wa mfumo wa kutengeneza mipango na mikakati ya pamoja ya uhifadhi wa simba, mikakati itakayosaida katika uwezeshaji wa uhifadhi wa simba na usimamizi, kukuza elimu katika jamii na kuanzishwa mfuko kwa ajili ya miradi ya dharurara.

- Zimeitaka CITES kuwasaidia katika uaandaaji wa uchambuzi yakinifu wa nchi ambazo zinaruhusu ama kutoruhusu uwindaji, kuwepo na fedha zitakazosaidia kujengwa kwa kikosi maalum cha CITES kuhusiana na simba ambacho kitajumuisha nchi ambazo zinaathiriwa zaidi na ujangili pamoja na biashara haramu na kufanya utafiti wa biashara haramu na halali ya simba pori, ikiwemo mifupa ya simba, kujua chimbuko na njia zinazotumika kupitisha biashara haramu na pia kutoa msaada kwa vyombo vya sharia



jameswarwick.co.uk

# ENDNOTES


[1] United Nations, Department of Economic and Social Affairs, Population Division (2015). World Population Prospects: The 2015 Revision, Key Findings and Advance Tables. ESA/P/WP.241. Retrieved from http://esa.un.org/unpd/wpp/publications/files/key_findings_wpp_2015.pdf

[2] Lindsey et al, in review 'Determinants of the effectiveness of African protected areas at conserving lions and their prey'

[3] African lion. (n.d.). Species Survival Commission Cat Specialist Group. Retrieved from http://www.catsg.org/index.php?id=108

[4] Rentsch, D. & Packer, C. (2012) Bushmeat consumption and local demand for wildlife: wildebeest offtake estimates for Western Serengeti. Unpublished Ph. D. Thesis. University of Minnesota, Saint Paul.

[5] Lindsey, P., Balme, G., Becker, M., Begg, C., Bento, C., Bocchino, C., Dickman, A., Diggle, R., Eves, H., Henschel, P., Lewis, D., Marnewick, K., Mattheus, J., McNutt, J.W., McRobb, R., Midlane, N., Milanzi, J., Morley, R., Murphree, M., Nyoni, P., Opyene, V., Phadima, J., Purchase, N., Rentsch, D., Roche, C., Shaw, J., van der Westhuizen, H., Van Vliet, N., Zisadza, P. (2015). Illegal hunting and the bush-meat trade in savanna Africa: drivers, impacts and solutions to address the problem. FAO/Panthera/Zoological Society of London/Wildlife Conservation Society report, New York. 79 pages.

[6] Vaughan, A. (2015). France bans imports of lion hunt trophies. Retrieved from http://www.theguardian.com/environment/2015/nov/19/france-bans-imports-of-lion-hunt-trophies

[7] Vaughan, A. (2015). UK to ban import of lion trophies if hunting industry doesn't reform. Retrieved from http://www.theguardian.com/environment/2015/nov/25/uk-to-ban-import-lion-trophies-if-hunting-industry-doesnt-reform

[8] Milman, O. (2015). Australia bans hunting 'trophies' from lions entering or leaving the country. Retrieved from https://www.theguardian.com/environment/2015/mar/13/australia-bans-hunting-trophies-from-lions-entering-or-leaving-the-country

[9] Cummings, W. (2015). Airlines ban hunters' big-game 'trophies' after uproar over Cecil the lion. Retrieved from http://www.usatoday.com/story/travel/flights/todayinthesky/2015/08/03/american-airlines-animal-trophy-ban/31090331/

[10] Batchelor, T. (2015). British Airways and Virgin pledge NEVER to carry big game trophies in wake of Cecil. Retrieved from http://www.express.co.uk/news/uk/595927/Cecil-lion-British-Airways-Virgin-ban-big-game-trophy-cargo

[11] Regulations.gov. (n.d.). Retrieved from https://www.regulations.gov/#!documentDetail;D=FWS-R9-ES-2012-0025-7055

[12] Platt, J. R. (n.d.). African Lions Finally Gain Endangered Species Act Protection. Retrieved from http://blogs.scientificamerican.com/extinction-countdown/african-lions-protection/

[13] Bauer, H., Packer, C., Funston, P. F., Henschel, P. & Nowell, K. (2015). Panthera leo. The IUCN Red List of Threatened Species 2015: e.T15951A79929984. http://dx.doi.org/10.2305/IUCN.UK.2015-4.RLTS.T15951A79929984.en

[14] Bauer, H., Chapron, G., Nowell, K., Henschel, P., Funston,P.,Hunter, L., Macdonald, D., & Packer, C . (2015). Lion (Panthera leo) populations are declining rapidly across Africa, except in intensively managed areas. Proc. Natl. Acad. Sci. 112, 14894–14899.

[15] Riggio, J. et al. (2015). Lion populations may be declining in Africa but not as Bauer et al. suggest. 10–11. doi:10.1073/pnas.1521506113

[16] Bauer, H., Packer, C., Funston, P. F., Henschel, P. & Nowell, K. (2015). Panthera leo. The IUCN Red List of Threatened Species 2015: e.T15951A79929984. http://dx.doi.org/10.2305/IUCN.UK.2015-4.RLTS.T15951A79929984.en

[17] CITES Animals Committee. (2015). Periodic Review of Panthera leo.

[18] Bauer, H., Packer, C., Funston, P. F., Henschel, P. & Nowell, K. (2015). Panthera leo. The IUCN Red List of Threatened Species.

[19] Henschel P, Coad L, Burton C, Chataigner B, Dunn A, MacDonald D, et al. (2014) The Lion in West Africa Is Critically Endangered. PLoS ONE 9(1): e83500. doi:10.1371/journal.pone.0083500

[20] Data | The World Bank. (n.d.). Retrieved from http://data.worldbank.org/

[21] United Nations, Department of Economic and Social Affairs, Population Division (2015). World Population Prospects: The 2015 Revision, Key Findings and Advance Tables. ESA/P/WP.241. Retrieved from http://esa.un.org/unpd/wpp/publications/files/key_findings_wpp_2015.pdf

[22] Endangered and Threatened Wildlife and Plants; Listing Two Lion Subspecies. (2015). Retrieved from https://www.federalregister.gov/articles/2015/12/23/2015-31958/endangered-and-threatened-wildlife-and-plants-listing-two-lion-subspecies#h-25

[23] Lindsey, P., Balme, G., Becker, M., Begg, C., Bento, C., Bocchino, C., Dickman, A., Diggle, R., Eves, H., Henschel, P., Lewis, D., Marnewick, K., Mattheus, J., McNutt, J.W., McRobb, R., Midlane, N., Milanzi, J., Morley, R., Murphree, M., Nyoni, P., Opyene, V., Phadima, J., Purchase, N., Rentsch, D., Roche, C., Shaw, J., van der Westhuizen, H., Van Vliet, N., Zisadza, P. (2015). Illegal hunting and the bush-meat trade in savanna Africa: drivers, impacts and solutions to address the problem. FAO/Panthera/Zoological Society of London/Wildlife Conservation Society report, New York. 79 pages.

[24] Chardonnet, P. et al. (2010). Managing the Conflicts Between People and Lion: Review and insights from the literature and field experience. Wildlife Management Working Paper 13. Food and Agriculture Organization of the United Nations Rome 2010. http://www.fao.org/docrep/012/k7292e/k7292e00.pdf

[25] Chardonnet, P. et al. Working Paper 13. Food and Agriculture Organization of the United Nations.

[26] Endangered and Threatened Wildlife and Plants; Listing Two Lion Subspecies. (2015). Retrieved from https://www.federalregister.gov/articles/2015/12/23/2015-31958/endangered-and-threatened-wildlife-and-plants-listing-two-lion-subspecies#h-25

[27] Lindsey et al, in review 'Determinants of the effectiveness of African protected areas at conserving lions and their prey'

[28] Lindsey, P. et al. Illegal hunting and the bush-meat trade in savanna Africa.

[29] Reduce Snaring. (n.d.). Retrieved from http://www.niassalion.org/reduce-snaring.php

[30] Lindsey, P. et al. Illegal hunting and the bush-meat trade in savanna Africa.

[31] Lindsey, P. et al. Illegal hunting and the bush-meat trade in savanna Africa.

[32] Lindsey, P. et al. Illegal hunting and the bush-meat trade in savanna Africa.

[33] Henschel, P., Hunter, L.T.B., Coad, L., Abernethy, K.A. & Mühlenberg, M. (2011) Leopard prey choice in the Congo Basin rainforest suggests exploitative competition with human bushmeat hunters. Journal of Zoology, 285, 11-20

[34] Lindsey, P., Balme, G., Becker, M., Begg, C., Bento, C., Bocchino, C., Dickman, A., Diggle, R., Eves, H., Henschel, P., Lewis, D., Marnewick, K., Mattheus, J., McNutt, J., McRobb, R., Midlane, N., Milanzi, J., Morley, R., Murphree, M., Opyene, V., Phadima, J., Purchase, G., Rentsch, D., Roche, C., Shaw, J., van der Westhuizen, H., Van Vliet, N., & Zisadza-Gandiwa, P. (2013). The bushmeat trade in African savannas: Impacts, drivers, and possible solutions. Biological Conservation 160:80-96.

[35] Lindsey et al. The bushmeat trade in African savannas.

[36] African lion. (n.d.). Species Survival Commission Cat Specialist Group. Retrieved from http://www.catsg.org/index.php?id=108

[37] Lindsey et al. The bushmeat trade in African savannas.

[38] Lindsey et al. The bushmeat trade in African savannas.

[39] African lion. (n.d.). Species Survival Commission Cat Specialist Group. Retrieved from http://www.catsg.org/index.php?id=108

[40] Lindsey, P. et al. Illegal hunting and the bush-meat trade in savanna Africa.

[41] Rentsch, D. & Packer, C. (2012) Bushmeat consumption and local demand for wildlife: wildebeest offtake estimates for Western Serengeti. Unpublished Ph. D. Thesis. University of Minnesota, Saint Paul.

[42] Lindsey, P. et al. Illegal hunting and the bush-meat trade in savanna Africa.

[43] New campaign targets snares in effort to save world's big cats. (2012). Retrieved from https://news.mongabay.com/2012/06/new-campaign-targets-snares-in-effort-to-save-worlds-big-cats/

[44] Henschel, P., Coad, L., Burton, C., Chataigner, B., Dunn, A., MacDonald, D., Saidu, Y. & Hunter, L.T.B. (2014) The lion in West Africa Is Critically Endangered. PLoS ONE, 9, e83500

[45] Williams, V. L., Newton, D. J., Loveridge, A. J. and Macdonald, D. W. (2015), Bones of contention: an assessment of the South African trade in African lion Panthera Leo bones and other body parts, 128 pages, TRAFFIC, Cambridge, UK & WildCRU, Oxford, UK

[46] Convention on International Trade in Endangered Species of Wild Fauna and Flora. Twenty-seventh meeting of the Animals Committee, Veracruz. (2014). Panthera Leo – Report of Kenya and Namibia. Retrieved from: http://www.cms.int/sites/default/files/document/ac27_cites_periodic_rev_status_african_lion_across_range_e.pdf

[47] Roberts, A. (2011). Conservation Risks and Threats to the Lion. Retrieved from http://www.bornfreeusa.org/articles.php?p=2729

[48] Endangered and Threatened Wildlife and Plants; Listing Two Lion Subspecies. (2015). Retrieved from https://www.federalregister.gov/articles/2015/12/23/2015-31958/endangered-and-threatened-wildlife-and-plants-listing-two-lion-subspecies#h-25

[49] China Outlaws the Eating of Tiger Penis, Rhino Horn, and Other Endangered Animal Products | VICE News. (n.d.). Retrieved from https://news.vice.com/article/china-outlaws-the-eating-of-tiger-penis-rhino-horn-and-other-endangered-animal-products

[50] Endangered and Threatened Wildlife and Plants; Listing Two Lion Subspecies. (2015). Retrieved from https://www.federalregister.gov/articles/2015/12/23/2015-31958/endangered-and-threatened-wildlife-and-plants-listing-two-lion-subspecies#h-25

[51] Bauer, H., Packer, C., Funston, P.F., Henschel, P. & Nowell, K. 2015. Panthera leo. The IUCN Red List of Threatened Species 2015: e.T15951A79929984. Retrieved from http://dx.doi.org/10.2305/IUCN.UK.2015-4.RLTS.T15951A79929984.en.

[52] Lindsey et al, in review 'Determinants of the effectiveness of African protected areas at conserving lions and their prey'

[53] African lion. (n.d.). Species Survival Commission Cat Specialist Group. Retrieved from http://www.catsg.org/index.php?id=108

[54] Lion King: Berkeley Carnivore Research Works to Halt the Decline of African Predators. (n.d.). Retrieved from http://alumni.berkeley.edu/california-magazine/january-february-2009-effect-change/lion-king-berkeley-carnivore-research-works

[55] Patterson, B., Kasiki, S., Selempo, E., & Kays, R. (2004). Livestock predation by lions (Panthera leo) and other carnivores on ranches neighboring Tsavo National Parks, Kenya. Biological Conservation 119: 507-516.

[56] Bauer, H., de Iongh, H. (2005). Lion (Panthera leo) home ranges and livestock conflicts in Waza National Park, Cameroon. African Journal of Ecology.

[57] Chardonnet, P. et al. (2010). Managing the Conflicts Between People and Lion: Review and insights from the literature and field experience. Wildlife Management Working Paper 13. Food and Agriculture Organization of the United Nations, Rome 2010.

[58] Frank, L., Hemson, G., Kushnir, H. and C. Packer. 2005b. Lions, conflict and conservation. Background paper, Eastern and Southern African Lion Conservation Workshop, Johannesburg, 8-13 January 2006.

[59] Frank, L. Maclennan, S., Hazzah, L. Bonham. R., & Hill, T., 2006 Lion Killing in the Amboseli-Tsavo Ecosystem, 2001-2006, and its Implications for Kenya's Lion Population, unpublished report.

[60] Frank, L., Hemson, G., Kushnir, H. and C. Packer. 2005b. Lions, conflict and conservation. Background paper, Eastern and Southern African Lion Conservation Workshop, Johannesburg, 8-13 January 2006.

[61] Creel, S., M'soka, J., Dröge, E., Rosenblatt, E., Becker, M., Matandiko, W., & Simpamba, T. (2016). Assessing the sustainability of African lion trophy hunting, with recommendations for policy. Ecological Applications. DOI: 10.1002/eap.1377.

[62] Steyn, P. Is Captive Lion Hunting Really Helping to Save the Species? (2015). Retrieved from http://news.nationalgeographic.com/2015/05/150504-lions-trophy-hunting-tiger-ban-south-africa-australia-cites/

[63] Lindsey, P., Alexander, R., Balme, G., Midlane, N., & Craig, J. Possible Relationships between the South African Captive-Bred Lion Hunting Industry and the Hunting and Conservation of Lions Elsewhere in Africa. (2012). South African Journal of Wildlife Research. Retrieved from http://www.bioone.org/doi/abs/10.3957/056.042.0103

[64] Williams, V.L., Newton, D.J., Loveridge, A.J. and Macdonald, D.W. (2015). Bones of Contention: An Assessment of the South African Trade in African Lion Panthera leo Bones and Other Body Parts. TRAFFIC, Cambridge, UK & WildCRU, Oxford, UK.

[65] Barkham, P. (2013). 'Canned hunting': The lions bred for slaughter. Retrieved from http://www.theguardian.com/environment/2013/jun/03/canned-hunting-lions-bred-slaughter

[66] Lindsey et al, in review. 'Determinants of the effectiveness of African protected areas at conserving lions and their prey'

[67] Lindsey, P. A., Balme, G. A., Funston, P. J., H. Henschel, P. and Hunter, L. T.B. (2016). Life after Cecil: channelling global outrage into funding for conservation in Africa, 2015. Conservation Letters. doi: 10.1111/conl.12224. Retrieved from http://onlinelibrary.wiley.com/doi/10.1111/conl.12224/full

[68] Packer et al. 2013 Conserving Large Carnivores: Dollars and Fence. Ecology Letters. doi: 10.1111/ele.12091.

[69] Packer et al. 2013 Conserving Large Carnivores: Dollars and Fence. Ecology Letters. doi: 10.1111/ele.12091.

[70] Lindsey, P., Balme, G., Madzikanda, H., Midlane, N., Hunter, L. (2013). The trophy hunting of African lions: current practices impeding sustainability. PLoS ONE DOI: 10.1371/journal.pone.0073808

[71] Creel, S., M'soka, J., Dröge, E., Rosenblatt, E., Becker, M., Matandiko, W., & Simpamba, T. (2016). Assessing the sustainability of African lion trophy hunting, with recommendations for policy. Ecological Applications. DOI: 10.1002/eap.1377

[72] CITES (n.d.). African Lion Range State Meeting. Retrieved from https://cites.org/sites/default/files/eng/news/pr/2016/African_Lion_Meeting_communique.pdf

PANTHERA

WILDAID

WILDCRU
Wildlife Conservation Research Unit